



SIKU YA NYWILA DUNIANI

Siku ya Nywila Duniani huadhimishwa Alhamisi ya kwanza ya mwezi Mei kila mwaka. Kwa mwaka 2021 maadhamisho ya Siku ya Nywila Duniani ni tarehe 6 Mei, 2021 na kauli mbiu ya mwaka huu ni “Umuhimu wa Nywila Thabiti”. Hii inamaanisha kuongeza uthibitishaji wenye nguvu kwa nywila zako muhimu ili kuzuia wizi wa utambulisho na uhalifu mwingine wa mtandaoni.

KWANINI SIKU YA NYWILA DUNIANI NI MUHIMU?

1. Kuna habari nyingi mtandaoni

Habari zetu nyingi zinaishi kwenye tovuti. Fikiria tu juu ya akaunti yako ya pesa mtandao, kurasa za mitandao ya kijamii, akaunti za benki mtandao, tovuti za ununuzi, na kadhalika. Hakikisha nywila ni ngumu na ambayo si rahisi mtu kukisia.

2. Faragha ni muhimu

Usimpe mtu yejote nywila yako, hata watu wa familia yako kwasababu mtu anapofanya kosa la jinai kupitia simu yako utawajibishwa wewe na sio yeye kwa sababu tu simu iliyotumiwa ni yako. Leo ni siku nzuri ya kukaa chini na kuijelimisha juu ya kwanini nywila iliundwa.

3. Kuna jambo la kujifunza

Zama za kuandika nywila kwenye karatasi zimepita. Swali ambalo unapaswa kujiuliza leo ni; Je! Unawekaje nywila yako salama? Tutumie siku hii kuhakikisha tunaweka nywila salama!